# ELOHIM SECONDARY SCHOOL

**P.O.BOX 580 Tanga. Cel: +255 (0) 717 018 283 / +255 (0) 621 110 563**

**Email: elohimeducation@yahoo.com**

**Website: www.elohim.ac.tz**

## MAELEZO YA KUJIUNGA NA KOZI YA MAANDALIZI YA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2026.

Kozi ya maandalizi ya kidato cha kwanza inaanza rasmi hapa shuleni mnamo tarehe **20/09/2025** Mpaka tarehe **06/12/2025** Kozi hii fupi ina malengo ya kumuandaa mwanafunzi katika mambo makuu matatu.

1. Kufanya marudio ya mambo muhimu aliyotakiwa kujifunza akiwa shule ya msingi.
2. Kufundishwa sheria zote za shule na kuzoeshwa ratiba nzima ya shule.
3. Kujifunza taratibu zetu za kufundisha na kujifunza hapa shuleni.
4. Kuanza masomo ya kidato cha kwanza.

Hivyo basi wazazi wote wenye wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza wanatakiwa kuhakikisha wanawaandaa watoto kufika shuleni katika muda muafaka.

Gharama za kozi ya maandalizi ya kidato cha kwanza ni shilingi **200,000/=.) MALIPO** YAFANYIKE KUPITIA AKAUNTI **NAMBA NMB 41710012288 ELOHIM PTA FUND.**

**Mwanafunzi atapaswa kuja na vifaa vifuatavyo katika kozi ya maandalizi ya kidato cha kwanza.**

a) Godoro lenya foronya ft 6 x upana ft 2 ½ x unene inch 4.
b) Viatu vyeusi vya ngozi jozi moja.
c) Soksi nyeupe zisizopungua jozi tatu zisiwe na urembo wowote.
d) Sanduku lenye usalama na lisiwe kubwa sana.
e) Taulo, daftari kubwa 5 (msomi), kalamu, mkebe wa geometry, penseli, rula, kifutio, sabuni ya kufulia na kuogea, dawa ya meno, mafuta ya kujipaka, mswaki.
f) Shuka mbili za blue bahari (3*6) kwa wavulana, pink kwa wasichana
g) Chandarua (3*6)
h) Kanda mbili za bafuni
i) Viatu vya wazi (Sandoz) (visiwe vya plastiki kama yeboyebo) na kwa wasichana visiwe na visingino virefu.
j) Sare zake za shule ya msingi.
k) Nguo za kushindia jozi mbili.
l) Ndoo.
m) Kanga doti 1 na kitenge doti 1(kwa wasichana)
n) Advance dictionary (Oxford) na Kamusi.
o) Fedha taslimu 6000/= kwa ajili ya vifaa vya kulia chakula.

Tunawatakia maandalizi mema.

**REV. DANIEL ANDREA MWARABU**
**MKUU WA SHULE.**

DOWNLOADED